# MIAKA MITATU (3) YA RAIS SAMIA SULUHU HASSAN HALMASHAURI YA WILAYA YA KASULU



## JARIDA MAALUM LA HALMASHAURI







www.kasuludc.go.tz

# UTANGULIZI

Mnamo Machi 19, 2024 Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan alitimiza miaka mitatu ya uongozi wake tokea alipoanza kuitumikia nafasi hiyo.

Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Thobias Andengenye hivi karibuni katika maadhimisho ya kilele cha Siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika kimkoa katika Kata ya Makere iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu alisema kuwa katika kipindi cha miaka hiyo mitatu wamepokea fedha kiasi cha shilingi trilioni 11.450 kutoka kwa Mama.

Fedha ambazo zimesaidia kuupaisha mkoa wetu pamoja na halmashauri zake kuondokana na changamoto lukuki zilizokuwepo hapo awali kitu kilichopelekea mkoa huo uonekane nyuma linapotamkwa suala la maendeleo.

Katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu katika miaka mitatu ya uongozi wake tumeshuhudia mambo mengi makubwa yakifanyika na kusaidia wilaya yetu kupaa zaidi ikiwemo kuvutia wawekezaji wenye mitaji mikubwa.

Wana Kasulu DC kwa kauli moja tunasema uongozi wako umeonesha kwa vitendo uwezo na umahiri walionao wanawake hasa linapokuja suala la kuwaletea maendeleo watu anaowaongoza.

Hakika hivi sasa kupitia uongozi wako mahiri hatuoni aibu kujinasibu kwamba tunatokea Mkoa wa Kigoma na kikubwa zaidi ni namna dunia nzima inavyotupia jicho nchi yetu kuangalia ni namna gani Rais wetu ulivyoweza  kufanya mambo yote makubwa tena kwa kipindi kifupi.

# WAHUSIKA

Jarida hili limeandaliwa na kutolewa na Kitengo cha Habari na Mawasiliano Serikalini.

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano Serikalini Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu,
**Alfred Lukonge**

Afisa Habari Kitengo cha Habari na Mawasiliano Serikalini,
**Twisile Nganga**

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu,
**George Msonge**

Msanifu Kurasa,
**Erick Esrom Chirandi**

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu
S.L.P 97,
Kasulu- Kigoma
**Simu Na. +255 028 2810339**
**Fax Na. +255 028 2810339**
**Baruapepe: ded@kasuludc.go.tz**
**Tovuti :www.kasuludc.go.tz**

# YALIYOMO

Utangulizi....................................................................................................2
Wahusika......................................................................................................3
Yaliyomo.......................................................................................................4
Ujenzi wa jengo la Makao Makuu..................................................................5
Ujenzi wa nyumba ya Mkurugenzi na Wakuu wa Idara...................................6
Sekta ya kilimo..............................................................................................7
Ujenzi wa soko la kisasa la mazao Nyakitonto................................................9
Sekta ya Elimu..............................................................................................10
Sekta ya Afya................................................................................................12
Maendeleo ya Jamii.......................................................................................14

# UJENZI WA JENGO LA MAKAO MAKUU

Katika kipindi cha miaka mitatu serikali imetoa fedha kiasi cha shilingi bilioni 3.065 kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi wa jengo la makao makuu ya halmashauri.

Jengo linalojumuisha ujenzi wa ofisi mbalimbali za idara na vitengo, sehemu ya kupokea wageni, jengo la walinzi, uzio pamoja na kantini.

Uwepo wa jengo hili umesaidia halmashauri kuhamia katika jengo lake la utawala kitu kitakachochea uendelezwaji wa eneo husika na kuongeza molari ya ufanyaji kazi kwa watumishi kutokana uhakika wa usalama ofisini.

Miundombinu bora inayopatikana katika jengo hili umesaidia kuwahudumia wananchi wote kwa urahisi ikiwemo hata wale wenye ulemavu.




*Picha mbalimbali zikionyesha mandhari ya jengo hilo la kisasa la halmashauri na viunga vyake lililogharimu kiasi cha shilingi bilioni 3.065 zilizotoka serikali kuu ili kuboresha utoaji huduma kwa wananchi.*

# UJENZI WA NYUMBA YA MKURUGENZI NA WAKUU WA IDARA

Katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi mahiri wa Mama Samia halmashauri imepokea shilingi milioni 150 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya Mkurugenzi na nyumba mbili za wakuu wa idara zenye thamani ya shilingi milioni 120.

Ujenzi wa nyumba ya Mkurugenzi itakapokamilika itamwezesha kuwa na makazi bora karibu na ofisi hivyo kutekeleza majukumu yake ipasavyo katika kuwahudumia wananchi. Kwa wakuu wa idara zitawasaidia kujituma katika ufanyaji kazi wao pamoja na kumaliza changamoto ya umbali kutoka katika makazi wanayoishi hivi sasa hadi zilipo ofisi za halmashauri.



*Moja kati ya nyumba mbili za wakuu wa idara zilizojengwa.*

# SEKTA YA KILIMO

Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB) na Mfuko wa Kusaidia Usalama wa Chakula (GAFSP) umefanikisha ujenzi wa ghala la kisasa la Nyakitonto lililogharimu kiasi cha shilingi bilioni 1.1 lenye uwezo wa kukusanya mazao ya nafaka tani 2000.

Uwepo wa ghala hilo utasaidia wakazi wa Kijiji cha Nyakitonto na vijiji jirani kuepukana na wadudu waharibifu, kukabiliana na sumu kuvu pamoja na uhakika wa soko huku kwa halmashauri kikiwa ni chanzo cha uhakika cha ukusanyaji wa mapato.

Vilevile wananchi kutoka makundi ya wasafirishaji, wafanyabiashara na wachakataji wa mazao wameanza kunufaika na mafunzo yanayotolewa na serikali juu ya namna ya kukabiliana na uchafuzi wa mazao.

Pia, kumekuwa na uendeshwaji wa mafunzo ya utengenezaji wa vienge vya chuma kama njia mojawapo ya kuwapa weledi wakulima jinsi ya kupambana na wadudu waharibifu baada ya mavuno.





*Picha mbalimbali zikionesha mwonekano wa ghala hilo pamoja na viambata vyake.*

# UJENZI WA SOKO LA KISASA LA MAZAO LA NYAKITONTO

Serikali kwa kushirikiana na Wakala wa Maendeleo wa Ubelgiji (Enabel) umetekeleza ujenzi wa mabanda 10 ya soko jipya la mazao la Nyakitonto na tayari awamu ya kwanza ya mradi iliyogharimu shilingi bilioni 1.18 imeshakamilika kwa 100%.

Uwepo wa soko hili utasaidia halmashauri kuongeza mapato pamoja na wakulima kuwa na uhakika wa soko baada ya mavuno.

# SEKTA YA ELIMU

Katika miaka mitatu ya Mama Samia shilingi bilioni 1.59 zimetolewa katika Idara ya Elimu Msingi na Awali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Boost.

Fedha hizi zimesaidia upatikanaji wa matundu 61 ya vyoo, madarasa 49,madarasa sita ya mfano, majengo mawili ya utawala pamoja na shule mpya mbili za Songambele na Mwitiri.

Ujenzi wa miundombinu hii mashuleni umesaidia kuzuia magonjwa ya milipuko, kuboresha usafi wa mazingira, kupunguza mrundikano mashuleni, ufaulu kuongezeka,watoto kutotembea umbali mrefu pamoja na kuongeza morali ya ufundishaji kwa walimu kutokana na kufanya kazi katika mazingira yaliyo rafiki.






*Muonekano wa shule mpya ya msingi Songambele iliyogharimu shilingi milioni 365.05 iliyopo Kata ya Kagera Nkanda iliyosaidia kupunguza wimbi la mrundikano uliokuwepo katika shule mama ya Msingi Mvinza.*




*Moja ya madarasa ya mfano yaliyojengwa kupitia mradi wa Boost.*

Mama hajaishia hapo tu katika Idara ya Elimu Sekondari  ametoa kiasi cha shilingi bilioni 4.04  ili kuboresha miundombinu mbalimbali mashuleni.

Ambapo kupitia fedha hizo halmashauri imeweza kupata shule mpya ya Sekondari Kasasa, ujenzi wa nyumba ya walimu katika Shule ya Sekondari Kamuganza pamoja na ujenzi wa madarasa mapya, mabweni na matundu ya vyoo katika Shule ya Sekondari Kabagwe inayotarajia kuanza kupokea wanafunzi wa kidato cha tano.



*Muonekano wa shule mpya ya sekondari Kasasa iliyojengwa katika miaka mitatu toka Mama Samia alipoingia madarakani.*



*Muonekano wa nyumba ya walimu ya mbili kwa moja iliyogharimu kiasi cha shilingi milioni 110 kutoka serikali kuu katika Shule ya Sekondari Kamuganza.*

# SEKTA YA AFYA

Halmashauri imepanua wigo wa huduma za afya kutoka kuwa na zahanati 33 hadi 37, vituo vya afya nane kufikia 10 na vyumba vya upasuaji saba kitu kilichowasaidia wananchi kuepekuna na tatizo la kusafiri umbali mrefu kufuata huduma za matibabu.





*Picha za Kituo cha Afya Rungwe Mpya kilichogharimu shilingi milioni 400 hadi kukamilika kwake ambapo baadhi ya huduma zimeshaanza kutolewa kituoni hapo.*




*Muonekano wa chumba cha kisasa cha upasuaji katika Kituo cha Afya Nyenge.*

# MAENDELEO YA JAMII

Katika kipindi cha miaka mitatu ya Mama Samia Idara ya Maendeleo ya Jamii imeweza kutoa mikopo ya shilingi 1,078,627,931 iliyoelekezwa kwa vikundi vya wanawake shilingi 476,316,943, vijana shilingi 526,310,988 na watu wenye ulemavu shilingi 76,000,000.

Kati ya fedha hizi kiasi cha shilingi 130,000,000 ilitolewa kuwezesha vikundi vya vijana vitatu vyenye idadi ya watu 51 mikopo ya vifaa vya pikipiki ili kuweza kujiajiri katika sekta hiyo ya usafirishaji.





Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu
S.L.P 97, Kasulu- Kigoma
Simu Na. +255 028 2810339
Fax Na. +255 028 2810339
Baruapepe: ded@kasuludc.go.tz
Tovuti :www.kasuludc.go.tz